JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
**OFISI YA WAZIRI MKUU**
**SERA, BUNGE NA URATIBU**

# MWONGOZO WA USIMAMIZI WA TATHMINI NCHINI

**JUNI, 2024**



# YALIYOMO


**YALIYOMO** .......... i
**ORODHA YA VIFUPISHO** .......... ii
**DIBAJI** .......... iii
**SURA YA KWANZA** .......... 1
**UTANGULIZI** .......... 1
1.1 Chimbuko .......... 1
1.2 Umuhimu .......... 1
1.3 Malengo .......... 2
**SURA YA PILI** .......... 3
HALI YA USIMAMIZI WA TATHMINI NCHINI .......... 3
2.1 Tafsiri na Aina za Tathmini .......... 3
2.2 Hali ya Ufanyaji Tathmini .......... 3
2.3 Matumizi ya Matokeo ya Tathmini .......... 3
2.4 Changamoto za Utekelezaji na Usimamizi wa Tathmini .......... 4
**SURA YA TATU** .......... 5
**UTARATIBU WA USIMAMIZI WA TATHMINI** .......... 5
3.1 Uibuaji wa Tathmini za Afua za Maendeleo .......... 5
3.2 Vigezo vya Kuzingatia Katika uchambuzi wa Tathmini .......... 5
3.3 Uainisho wa Tathmini kwa Kuzingatia Vigezo; .......... 5
3.4 Vigezo vya Uchambuzi wa Tathmini – Ngazi ya Taifa .......... 5
3.5 Vigezo vya Uchambuzi wa Tathmini – Ngazi ya Sekta .......... 6
3.6 Uchambuzi na Uthibitishaji wa Utekelezaji wa Tathmini .......... 6
**SURA YA NNE** .......... 7
**MUUNDO NA MAJUKUMU YA USIMAMIZI WA TATHMINI** .......... 7
4.1 Muundo wa Usimamizi wa Tathmini .......... 7
4.2 Majukumu ya Usimamizi .......... 7
4.3 Usimamizi wa Tathmini - Kitaifa .......... 7
4.4 Usimamizi wa Tathmini – Wizara .......... 8
4.5 Usimamizi wa Tathmini – Idara Zinazojitegemea, Mamlaka na Wakala za Serikali 8
4.6 Ofisi ya Rais Tawala za Mikao na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) .......... 8
4.7 Sekretarieti za Mikoa .......... 9
4.8 Mamlaka za Serikali za Mitaa .......... 9

## ORODHA YA VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| **OWM – SBU** | Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Bunge na Uratibu |
| **OR – TAMISEMI** | Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali na Mitaa |
| **PMED** | Performance Monitoring and Evaluation Division |
| **TDV** | Tanzania Development Vision |
| **NAEP** | National Annual Evaluation Plan |
| **FYDP** | Five Years Developmment Plan |
| **SDGs** | Sustainable Development Goals |
| **OECD** | Organzanion for Economic Co-operation and Developments |



# DIBAJI

Kwa mujibu wa Ibara ya 52 (1) – (3) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, Waziri Mkuu ana mamlaka ya kudhibiti, kusimamia utekelezaji wa siku hata siku wa kazi na shughuli za Serikali ya Jamhuri ya Muungano. Mamlaka haya yanajenga msingi kwa Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Bunge na Uratibu (OWM – SBU) kusimamia ufuatiliaji, tathmini na utendaji wa afua zote za Serikali ambazo ni sera, mikakati, mipango, miradi, programu za maendeleo na shughuli zote za Serikali.

Kwa msingi huo, tathmini za afua za maendeleo zinafanyika kwa lengo la kupima utendaji wa serikali kwa kuzingatia vigezo vinavyokubalika kitaifa na kimataifa. Hivyo, tathmini hufanyika ili kupima utendaji na utekelezaji wa afua za maendeleo ambazo ni Sera, Mipango, Mikakati, Miradi, Programu na Miongozo katika kufikia Dira ya Taifa ya Maendeleo. Matokeo yatokanayo na tathmini hizo hulenga kusaidia katika kurekebisha na kuboresha usimamizi wa afua hizo. Kwa msingi huo, dhana ya tathmini ufungamanishwa na kujifunza (*evaluation for learning*).

Serikali imefanya jitihada mbalimbali uratibu wa tathmini nchini. Hatahivyo, katika utekelezaji wa shughuli za tathmini changamoto zifuatazo zimebainika: [1] Kutokuwepo kwa Mpango wa Tathmini; [2] Kufanyika mapitio ya afua mbalimbali kama vile Sera badala ya tathmini; [3] matokeo ya tathmini kutokutumika katika maandalizi ya mipango na ufanyaji wa maamuzi; [4] uwezo hafifu wa kitaalam katika kutekeleza kazi za tathmini. [5] mawanda ya tathmini kujielekeza kwenye miradi na programu na sio kwenye sera, mipango, mikakati na dira; na [6] mtazamo hasi kuhusu suala la tathmini mathalani kuonekana kuwa utekelezaji wake ni mgumu, unachukua muda na gharama.

Hivyo, Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Bunge na Uratibu imeandaa Mwongozo wa usimamizi wa shughuli za tathmini kwa lengo la kuelekeza utaratibu wa kuzingatia katika uibuaji, maandalizi, uchambuzi na matumizi ya matokeo ya tathmini. Aidha, malengo mahsusi ni kutoa maelekezo katika: Kuainisha vigezo vya kuzingatia katika uibuaji wa tathmini; Utaratibu wa usimamizi wa tathmini kwa ngazi zote za Serikali; na Kuainisha muundo wa kitaasisi utakaozingatiwa katika usimamizi wa tathmini kwa ngazi za Kitaifa na Kisekta.

Vilevile, Mwongozo unaainisha muundo wa usimamizi na majukumu ya kila taasisi kwa ngazi za kitaifa, kisekta na Wizara, Idara Zinazojitegemea, Mashirika ya Umma, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Majukumu hayo yanaainisha kazi zinazotakiwa kutekelezwa ili kuwezesha utekelezaji wa tathmini zilizopangwa kufanyika katika kipindi husika. Aidha, muundo huu utarahisisha uratibu wa shughuli za tathmini katika ngazi zote.

Hivyo, matumizi ya Mwongozo huu yatawezesha Serikali kusimamia utekelezaji wa tathmini za afua mbalimbali katika taasisi zote kuanzia ngazi ya kitaifa, kisekta na kujenga msingi wa uwazi na uwajibikaji wa taasisi husika katika kuleta mchango wa maendeleo na utoaji wa huduma kwa wananchi.

..........................................................................

***Mhe*. Jenista Joachim Mhagama (Mb)**
**Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu,**
**Sera Bunge na Uratibu**

SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.1 Chimbuko

Chimbuko la kufanya tathmini ya afua za maendeleo linatokana na dhana na upimaji wa utendaji na utekelezaji wa Sera, Mipango, Mikakati, Miradi, Programu na Miongozo katika kufikia Dira ya Taifa ya Maendeleo. Hii inamaanisha kuwa, kutokana na yanayobainika katika upimaji wa utekelezaji wa afua hizo, Taasisi za Umma zinawajibika kutumia yaliyobainika ili kurekebisha na kuboresha usimamizi wa afua hizo. Kwa msingi huo, dhana ya tathmini ufungamanishwa na kujifunza (*evaluation for learning*).

Kitaalamu, tathmini huzingatia vigezo sita (6) ambavyo ni: ufanisi, umuhimu, uendelevu, kufungamana na afua nyingine (*coherence*) na matokeo ya muda mrefu. Hata hivyo, vigezo hivyo hutumika kulingana na aina, malengo na umuhimu wa tathmini husika. Kulingana na Mwongozo Jumuishi wa Ufuatiliaji na Tathmini – 2024, zipo aina mbalimbali za tathmini zikijumuisha: tathmini za kizio (*baseline evaluation*), tathmini za ndani (*internal evaluation*) na tathmini huru (*external/independent evaluation*).

Kwa sasa ufanyaji wa tathmini umejielekeza katika baadhi ya miradi hususan ambayo hutekelezwa kwa fedha za wadau wa maendeleo. Hivyo, tathmini hizo zimekuwa zikifanyika kutokana na matakwa ya wadau wa maendeleo. Mathalani, baadhi ya sekta kama vile sekta za elimu, afya na maji zimekuwa zikifanya tathmini kwa lengo la kujenga hoja ya kuandaa programu na kupata fedha za utekelezaji kutoka kwa wadau.

Usimamizi na matokeo ya (*evaluation findings*) unatekelezwa kwa kutumia miongozo ya wadau husika. Hii inamaanisha kwamba hakuna utaratibu wa matumizi ya matokeo ya tathmini katika maboresho ya sera, mipango, miradi na programu zinazogharamiwa kwa fedha za ndani. Vile vile, miongozo mingi ya ufuatiliaji na tathmini imejielekeza katika eneo la ufuatiliaji hususan wa miradi. Hata hivyo, hakuna utaratibu wa usimamizi wa tathmini hizo.

Ijapokuwa Serikali imeendelea kuweka msisitizo katika kufanya tathmini, ni wazi kwamba utekelezaji wa tathmini ni mdogo sana ikilinganishwa na umuhimu wake na matokeo ya tathmini hazingatiwi vya kutosha katika kuboresha mipango, sera na mikakati ya maendeleo. Hali hii inatokana na gharama kubwa ya ufanyaji wa tathmini na kukosekana kwa muundo madhubuti wa usimamizi wa matokeo ya tathmini. Kwa msingi huo, ni muhimu kuwa na Mwongozo wa Tathmini utakaoeleza matumizi ya tathmini, muundo wa usimamizi wa tathmini na majukumu ya kila mdau katika ufanyaji tathmini.

## 1.2 Umuhimu

Kitalaamu, tathmini hujenga msingi wa kufanya maamuzi kuhusu mabadiliko ya  utekelezaji na usimamizi wa miradi, mipango, sera na mikakati. Hivyo, kutokuwa na uratibu mzuri wa matumizi ya tathmini husababisha kutkutumiwa kwa matokeo ya tathmini hizo au kuongezeka kwa maamuzi yasiyokuwa na misingi ya kitaalamu. Hii inajenga hoja kwa Serikali na wadau wengine wa maendeleo kuhusu kiwango cha matumizi ya matokeo ya tathmini katika maamuzi na athari zake pindi yasipotumiwa ka ufanisi.

Kukosekana kwa usimamizi wa matumizi ya matokeo ya tathmini kumesababisha taasisi nyingi za Serikali kujielekeza katika ufuatiliaji pekee. Hali hii inasababisha kuchelewa kuibuliwa kwa masuala ya kisera na kiutendaji na hivyo kupunguza thamani ya fedha iliyowekezwa katika afua husika. Kwa kuwa tathmini ndio msingi wa maamuzi hivyo ni muhimu kuweka utaratibu mahsusi wa kimuundo wa kuratibu ufanyaji wa tathmini, uchambuzi na matumizi yake katika kuishauri Serikali.

### 1.3 Malengo

Lengo kuu la Mwongozo wa Usimamizi wa Tathmini ni kuelekeza utaratibu wa kuzingatia katika uibuaji, maandalizi, uchambuzi na matumizi ya matokeo ya tathmini. Aidha, malengo mahsusi ni:

(i). Kuainisha vigezo vya kuzingatia katika uibuaji wa tathmini;
(ii). Utaratibu wa usimamizi wa tathmini kwa ngazi zote za Serikali;
(iii). Kuainisha muundo wa kitaasisi utakaozingatiwa katika usimamizi wa tathmini kwa ngazi za Kitaifa na Kisekta

# SURA YA PILI

## HALI YA USIMAMIZI WA TATHMINI NCHINI

Sura hii inaeleza kwa mapana kuhusu dhana usimamizi wa tathmini *(Managing Evaluations)* nchini kwa kuzingatia maeneo mahsusi yafuatayo: *[1]* tafsiri na aina za tathmini kwa lengo la kujenga uelewa sahihi na wa pamoja katika suala la utekelezaji wa tathmini kwa kuzingatia Mwongozo Jumuishi wa Ufuatiliaji na Tathmini *[2]* hali ilivyo ya ufanyaji wa Tathmini; *[3]* matumizi ya matokeo ya tathmini zinazofanyika; *[4]* changamoto za utekelezaji na usimamizi wa tathmini; *[5]* nyenzo wezeshi za usimamizi wa tathmini; *[6]* Muundo wa Usimamizi wa Tathmini na Masuala ya Usimamizi Yanayohitaji Mwongozo. Kimsingi eneo la usimamizi wa tathmini linahitaji utashi na utayari wa Wasimamizi wa Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Mashirika ya Umma, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ili matokeo ya tathmini hizo yatumike na kuleta tija katika utendaji wa Serikali.

### 2.1 Tafsiri na Aina za Tathmini

Tathmini uhusisha kupima na kuchunguza matokeo halisi ya muda mfupi au mrefu ya afua mbalimbali zilizotekelezwa zikijumuisha miradi, programu, mpango, mkakati na sera kwa lengo la kupata data zinazotoa ushahidi wa kutosha kwa menejimenti, kiongozi, mtawala au meneja kwa lengo la kufanya maboresho na maamuzi *(Informed and Evidence Based Decision Making).* Tathmini zinazofanyika kwenye afua mbalimbali hujenga msingi katika upimaji wa hali na hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa afua husika kwa kuzingatia vigezo maalumu vya ufanisi, umuhimu, uendelevu, kufungamana na afua nyingine (*coherence*) na matokeo ya muda mrefu. Zipo aina mbalimbali za tathmini zikijumuisha: tathmini za kizio (baseline evaluation/feasiblity study), tathmini za ndani (internal evaluation) na tathmini huru (external/independent evaluation).

Hivyo, usimamizi wa tathmini ufanyike kabla, wakati au mwishoni mwa afua kwa kuzingatia maeneo yafuatayo: *[1]* Kuhakikisha tathmini imefuata Mwongozo jumuishi wa Ufuatiliaji na Tathmini ikiwa ni pamoja vigezo vya kufanya tathmini *[2]* Kuhakikisha tathmini inafanyika kwa wakati uliopangwa kulingana na aina ya tathmini husika. *[3]* Kusimamia upatikanaji wa wahusika wa Tathmini kulingana na aina ya tathmini na *[4]* rasilimali fedha zinatengwa ili kuwezesha tathmini ifanyike kwa wakati [5] uzingatiaji wa Mbinu za Tathmini ili kufikia malengo tarajiwa *[6]* Kuwezesha matokeo ya tathmini yafikishwe kwa walaji na wafanya maamuzi *[7]* kusimamia matumizi ya takwimu kwa kusudi la kuboresha na kuimarisha utendaji wa taasisi.

### 2.2 Hali ya Ufanyaji Tathmini

Ufanyaji wa tathmini umejielekeza kwenye miradi, program, mipango, mikakati na sera mbalimbali. Uchache wa tathmini hizo unatokana na gharama kubwa ya ufanyaji wa tathmini na kutokuwepo kwa Mpango wa Taifa wa Tathmini wa Mwaka (*National Annual Evaluation Plan - NAEP*). Aidha, tathmini zinazopewa kipaumbele ni zile zinazohusisha miradi na program ambazo hupata ufadhili wa kifedha kutoka kwa wadau wa maendeleo. Hivyo, tathmini hizo zimekuwa zikifanyika kwa msukumo wa nje zaidi kwa kufuata matakwa ya wadau wa maendeleo badala ya msukumo wa ndani. Mathalani, baadhi ya sekta kama vile sekta za elimu, afya na maji zimekuwa zikifanya tathmini kwa lengo la kujenga hoja ya kuandaa programu na kupata fedha za utekelezaji kutoka kwa wadau. Baadhi ya tathmini ambazo zimefanyika ni pamoja na tathmini za Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji Awamu ya Kwanza (2009/10 – 2015/16) na Awamu ya Pili (2016/17 – 2021/22) na Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo Awamu ya Kwanza.

Vilevile, tathmini zinafanyika katika upimaji wa utekelezaji wa mipango, kama vile tathmini ya utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2016/17 – 2020/21 (FYDP II). Kadhalika, tathmini zimeendelea kufanyika katika upimaji wa utekelezaji wa sera za kisekta. Hii inatokana na maelekezo ya Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri katika kutekeleza Mwongozo wa Uandaaji wa Nyaraka za Baraza la Mawaziri wa Mwaka 2010 Toleo la Mwaka 2014.

Ijapokuwa Serikali imeendelea kuweka msisitizo katika kufanya tathmini, ni wazi kwamba utekelezaji wa tathmini ni mdogo sana ikilinganishwa na umuhimu wake. Hii husababisha kutokutumiwa kwa matokeo ya tathmini hizo katika maboresho ya mipango ya Serikali (re-planning), kuimarisha utekelezaji kutokana na matokeo ya tathmini (evaluation for learning) na kuongezeka kwa gharama za utekelezaji wa miradi kwa muda mrefu. Hali hii inatokana na gharama kubwa ya ufanyaji wa tathmini na kutokuwepo kwa Mpango wa Taifa wa Tathmini wa Mwaka (National Annual Evaluation Plan - NAEP). Aidha, uchambuzi unaonesha kuwa kwa nchi zilizoimarisha mifumo ya usimamizi wa utendaji kama vile Chile, Australia na Afrika Kusini wastani wa tathmini 12 hufanyika kwa mwaka. Hivyo ni muhimu kuwa na Mpango wa Taifa wa tathmini unaoainisha tathmini muhimu hususan za miradi ya kielelezo na kimkakati.

## 2.3 Matumizi ya Matokeo ya Tathmini

Matumizi hayo hutokana na matokeo yaliyobainishwa wakati wa kufanya tathmini ya afua zinazotekelezwa katika ngazi husika. Kimsingi, matumizi ya matokeo ya tathmini ni kwa lengo la kujifunza *(Learning from the insights obtained from evaluations)* kutokana na mrejesho wa utendaji wa afua husika. Umuhimu wa matumizi ya matokeo hayo ni kuboresha sera na sheria, kurekebisha mipango na mikakati, na kuboresha miradi na programu zinazotekelezwa. Aidha, kiutendaji matumizi ya matokeo ya tathmini hizo yanapaswa kutumika kuboresha na kuimarisha utendaji katika ngazi mbalimbali za kiutawala na kiutekelezaji zikijumuisha Halmashauri, Tawala za Mikoa, Taasisi, Wizara na Sekta. Maboresho hayo hutokea pale ambapo matokeo yanapokelewa kwa uchanya na wafanya maamuzi na kutumika katika utekelezaji wa afua mbalimbali. Hatahivyo, mapokeo ya matokeo ya tathmini yamekuwa yakipokelewa kama tishio kwa wafanya maamuzi serikalii ikilinganishwa na mapokeo ya matokeo husika kwa wadau wa maendeleo; matumizi yake ni hafifu; na hivyo kupelekea kuhifadhiwa kama kumbukumbu na sio kwa lengo la kutumika. Kutotumika kwa matokeo ya tathmini hushindwa kutoa mchango katika mipango, mikakati, sera, miradi na programu za kitaifa, kisekta, wizara na taasisi mbalimbali serikalini.

Hivyo, menejimenti ya taasisi husika inapaswa kutekeleza yafuatayo ili kuwezesha matumizi ya takwimu zinazozalishwa kutoka katika tathmini mbalimbali; [1] Kusimamia maandalizi ya nyenzo ya usimamizi wa takwimu ndani ya taasisi [2] kusimamia utamaduni wa matumizi ya takwimu (Data use culture) katika ufanyaji wa maamuzi [3] Kusimamia maandalizi na utekelezaji wa mkakati wa usambazaji wa takwimu [4] Kusimamia ujenzi wa mfumo wa kielektroniki utakaowezesha wafanya maamuzi kupata matokeo ya tathmini kwa wakati na kuyafanyia kazi [5] Kusimamia mafunzo ya kuwajengea uwezo wafanya maamuzi ili kujenga mtazamo chanya juu ya tathmini zinazofanyika.

## 2.4 Changamoto za Utekelezaji na Usimamizi wa Tathmini

Ufanyaji wa tathmini nchini ni hafifu na umegubikwa na ugumu katika utekelezaji na usimamizi na kupelekea changamoto zifuatazo: *[1]* Usimamizi hafifu wa ukusanyaji, uchakataji, uthibitishaji, tafsiri na matumizi ya data na takwimu; *[2]* Mitazamo hasi kuhusiana na kazi za tathmini kwa kuhofia uhaba wa rasilimali fedha, muda unaotumiwa kufanya tathmini hizo na kuibua udhaifu wa utendaji wa taasisi husika *[3]* Ushirikiano, uhusika na ushirikishwaji wa kazi za tathmini kati ya Maofisa wataalam wanaofanya kazi za tathmini na menejimenti za taasisi kuwa hafifu *[4]* kubadilika kwa data mara kwa mara kwa lengo la kuwaridhisha watoa maamuzi, hii hutokana na mtazamo kuwa data ikiwa ya kweli inahatarisha nafasi ya Mkuu wa Taasisi, Idara au Afisa masuuli wa Wizara husika *[5]* Kukosa nyenzo muhimu za usimamizi wa tathmini ndani ya serikali.

SURA YA TATU

# UTARATIBU WA USIMAMIZI WA TATHMINI

Sura hii inaeleza utaratibu utakaofuatwa katika: Uibuaji wa Tathmini za Afua za Maendeleo; Vigezo vya kuzingatia katika uchambuzi wa Tathmini; Uainisho wa Tathmini kwa kuzingatia Vigezo; Uchambuzi na Uthibitishaji wa Utekelezaji wa Tathmini.

## 3.1 Uibuaji wa Tathmini za Afua za Maendeleo

Uibuaji wa tathmini za afua za maendeleo unazingatia muda wa utekelezaji, shughuli au kazi zilizokamilishwa, umuhimu wa tathmini husika kwa kuzingatia mahitaji na athari za kutokufanya tathmini hiyo kwa wakati huo. Kiutekelezaji, uibuaji wa tathmini ufuate hatua zifuatazo:

i. Ainisha afua zote ambazo zitafanyiwa tathmini. Afua hizo zinajumuisha mipango, mikakati, miradi, miongozo na programu;
ii. Zingatia muda husika wa afua mahsusi ili kuifanya tathmini kuwa ya tija;
iii. Wasiliana na Idara/Kitengo husika kuhusu tathmini hiyo;
iv. Fanya kikao cha pamoja kuhusu afua na tathmini husika kwa ajili ya kujenga uelewa na wadau wote; na
v. Fungamanisha tathmini husika na Miongozo ya Taifa ya Maendeleo ikijumuisha TDV, FYDPs na SDGs.

## 3.2 Vigezo vya Kuzingatia katika uchambuzi wa Tathmini

Katika uchambuzi wa tathmini, Idara izingatie vigezo vya kitaalamu na utaratibu wa utekelezaji wa tathmini husika. Vigezo hivi visichanganywe na vile vya kitaalamu ambavyo vimetolewa na OECD. Kwa msingi huo vigezo vya kuzingatia katika uchambuzi wa tathmini ni:

i. Andiko dhana linaloeleza usuli, msingi, umuhimu na malengo ya tathmini husika;
ii. Andiko dhana liambatishwe na takwimu na uchambuzi wa kutosha kuwezesha ulinganifu wa umuhimu wa tathmini husika;
iii. Andiko liwasilishwe katika kitengo cha ufuatiliaji na tathmini cha Taasisi husika kwa ajili ya kuchambuliwa kwa kuzingatia maelezo ya (i);
iv. Uchambuzi wa andiko uwasilishwe OWM-SBU – Idara ya PMED kwa ajili ya uidhinishaji na kutoa ruhusa ya maandalizi ya andiko la tathmini (*evaluation doc.*).

## 3.3 Uainisho wa Tathmini kwa Kuzingatia Vigezo;

Uanishaji wa tathmini utazingatia umuhimu wa tathmini husika kwa ngazi ya sekta na Taifa. Aidha, tofauti ya tathmini hizo inajengeka katika msingi wa kufungamanisha sekta kwa kutumia mipango ya sekta au kufikia malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo. Mchanganuo wa vigezo hivyo unatolewa katika mwongozo huu na usimamizi wake unajumuisha Ofisi ya Waziri Mkuu – SBU, Idara ya Ufuatiliaji na Tathmini kwa ngazi ya Kitaifa na vitengo vya U&T ngazi ya Wizara, Sekretarieti ya Mikoa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa.

## 3.4 Vigezo vya Uchambuzi wa Tathmini – Ngazi ya Taifa

Kwa ngazi ya Taifa, tathmini italenga kuakisi matokeo ya muda mrefu (impact) kwa kufungamanishwa na Dira ya Taifa ya Maendeleo kwa wakati huo. Aidha, tathmini hiyo izingatie vigezo mahsusi kama ifuatavyo:-

i. Kuwepo katika Mpango wa Taifa wa Tathmini wa Mwaka husika (National Evaluation Plan). Mpango huo uandaliwe na Ofisi ya Waziri Mkuu – SBU Idara ya Ufuatialiaji na Tathmini ya Shughuli za Utendaji wa Serikali .

ii. Msingi wa tathmini uwe ni afua za maendeleo za kielelezo (Flagship Development interventions) kama vile miradi ya kielelezo, Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Muda wa Kati (FYDPs) na Dira ya Taifa ya Maendeleo (TDV).

iii. Kufungamanishwa na miongozo ya maendeleo ya kimataifa kama vile Malengo ya Maendeleo Endelevu SDG 2030 na Agenda 2063 – The Africa we want.

### 3.5 Vigezo vya Uchambuzi wa Tathmini – Ngazi ya Sekta

Kwa ngazi ya Sekta, tathmini zitalenga kuakisi matokeo ya muda wa kati kwa sekta husika kwa kufungamanisha na mipango, mikakati na programu za sekta. Tathmini hizo zizingatie vigezo vifuatavyo;-

i. Kuwepo katika Mpango wa tathmini wa Wizara, Sekretarieti ya Mkoa, Mamlaka ya Serikali za Mitaa au Taasisi husika (Annual Evaluation Plan)

ii. Msingi wa tathmini hiyo uwe ni kuendelea au kumalizika kwa mradi, programu au mkakati kwa ngazi ya sekta

iii. Kuakisi mchango wa tathmini hiyo katika miongozo ya Kitaifa kama vile TDV na kimataifa kama vile Malengo ya Maendeleo Endelevu SDG 2030 na Agenda 2063 – The Africa we want.

### 3.6 Uchambuzi na Uthibitishaji wa Utekelezaji wa Tathmini

Uchambuzi uzingatie vigezo vilivyoainishwa katika sehemu 3.3. Aidha, Idara, Sehemu au Vitengo simamizi vya masuala ya ufuatiliaji na tathmini zizingatie hatua za kitaalamu za tathmini kama zilivyoainishwa katika Mwongozo Jumuishi wa Ufuatiliaji na Tathmini – 2024. Kwa msingi huo,

i. Uthibitishaji wa Utekelezaji wa Tathmini utasimamiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Bunge na Uratibu kupitia Idara ya Ufuatiliaji na Tathmini ya Utendaji wa Serikali.

ii. Hivyo, taasisi zote za Serikali bila kuzingatia ngazi au aina ya taasisi zitawajibika kupitisha maandiko ya tathmini (*andiko dhana, andiko la tathmini* na *taarifa za tathmini*) katika Sehemu au Vitengo vinavyohusika na tathmini ili kupata idhini ya kuwasilisha OWM-SBU ili kuthibitishwa kwa ajili ya utekelezaji.

SURA YA NNE

# MUUNDO NA MAJUKUMU YA USIMAMIZI WA TATHMINI

Sura hii inaeleza muundo na majukumu ya usimamizi wa shughuli za tathmini katika Idara, vitengo na sehemu za ufuatiliaji na tathmini kuanzia ngazi za Mamlaka za Serikali za Mtaa hadi ngazi ya Taifa. Vilevile, sura inaainisha majukumu ya wadau mbalimbali katika usimamizi wa tathmini kwenye maeneo ya mbalimbali ya kiutendaji.

## 4.1 Muundo wa Usimamizi wa Tathmini

Muundo wa usimamizi wa tathmini unatokana na miongozo elekezi. Kitaifa, ***Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Bunge na Uratibu (OWM-SBU)*** kupitia Idara ya Ufuatiliaji na Tathmini ya Utendaji wa Shughuli za Serikali inasimamia utekelezaji tathmini zilizopangwa kwa vipindi mbalimbali. Mgawanyo wa majukumu ya usimamizi kwa ngazi mbalimbali ni kama ifuatavyo:-

(i). Katika ngazi ya Taifa, Idara ya Ufuatiliaji na Tathmini ya Utendaji wa Shughuli za Serikali iliyopo Ofisi ya Waziri Mkuu – SBU itasimamia ubora wa mipango ya tathmini katika ngazi za Wizara, Taasisi, Wakala za Serikali na Idara Zinazojitegemea.

(ii). Katika ngazi ya Wizara za kisekta na taasisi, usimamizi wa tathmini utafanywa na vitengo au sehemu inayohusika na ufuatiliaji na tathmini. Vitengo au Sehemu hizo zitawajibika kuandaa Mpango wa tathmini katika sekta na kuiwasilisha kwenye Menejimenti ya Wizara kwa ajili ya maoni; kuiwasilisha Ofisi ya Waziri Mkuu kwa ajili ya mapitio na ikipitishwa ianze kutekelezwa.

(iii). Kwa upande wa Sekretarieti za Mikoa, jukumu la usimamizi wa tathmini linatekelezwa kupitia Sehemu ya Mipango na Uratibu na kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa jukumu hili linafanyika kupitia Idara ya Mipango na Uratibu.

## 4.2 Majukumu ya Usimamizi

Majukumu ya usimamizi wa tathmini yameainishwa kwa kuzingatia ngazi mbalimbali za kiutendaji na utawala nchini. Majukumu hayo yamegawanywa katika ngazi ya kitaifa, Wizara, Idara Zinazojitegemea, Mamlaka na Wakala za Serikali, OR-TAMISEMI, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mtaa.

## 4.3 Usimamizi wa Tathmini - Kitaifa

Kitaifa, Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Bunge na Uratibu ni msimamizi mkuu wa tathmini zote zinazoandaliwa na kutekelezwa katika ngazi zote Serikalini. Usimamizi wa tathmini hizo utafanyika kupitia Idara ya Ufuatiliaji na Tathmini ya Utendaji wa Serikali. Aidha, katika kusimamia utekelezaji wa tathmini hizo, Idara itawajibika na:

(i). Kusimamia ubora wa tathmini za afua za maendeleo kwa taasisi zote za Serikali
(ii). Kusimamia maandalizi ya nyenzo zitakazotumika kufanya tathmini
(iii). Kuhakikisha vigezo vinavyotumika katika aina za tathmini zinazotekelezwa vinafuatwa.
(iv). Kusimamia uchambuzi na uchakataji wa tathmini zitakazotekelezwa
(v). Kusimamia maandalizi ya mpango wa tathmini wa mwaka; na
(vi). Kuidhinisha mipango ya tathmini (*evaluation plans*) ya taasisi zote za Serikali
(vii). Kusimamia utekelezaji wa mapendekezo yanayotokana na matokeo ya tathmini hizo.
(viii). Kusimamia na kuratibu ujenzi wa uwezo wa kufanya tathmini za afua mbalimbali

## 4.4 Usimamizi wa Tathmini – Wizara

Vitengo vya Ufuatiliaji na Tathmini vitawajibika kusimamia tathmini zinazopaswa kutekelezwa katika Taasisi, idara, vitengo na sehemu zilizochini yake. Katika kutekeleza hilo, vitengo hivyo vitawajibika:

(i). Kusimamia Idara, vitengo na sehemu zilizo chini ya Wizara katika maandalizi ya Mpango wa Tathmini wa Wizara husika na Taasisi zake.
(ii). Kusimamia utekelezaji wa tathmini hizo kulingana na wakati uliopangwa
(iii). Kusimamia matumizi ya matokeo ya tathmini kwa lengo la kufanya maboresho, kufanya maamuzi yenye ushahidi na kujifunza.
(iv). Kusimamia ubora wa data na takwimu zinazotokana na tathmini za wizara na taasisi zake;
(v). Kuandaa nyenzo mahsusi za ufuatiliaji wa Wizara kulingana na maelekezo ya Mwongozo;

## 4.5 Usimamizi wa Tathmini – Idara Zinazojitegemea, Mamlaka na Wakala za Serikali

Usimamizi wa tathmini kwa Idara Zinazojitegemea, Mamlaka na Wakala za Serikali unategemeana na muundo wa taasisi hizo. Aidha, kwa muktadha wa Mwongozo huu Idara/Sehemu/Kitengo kitakachohusika na jukumu hilo kitatekeleza kazi zifuatazo:

(i). Kusimamia maandalizi ya Mpango wa tathmini wa taasisi na kuuwasilisha wizara husika kwa ajili ya kuidhinishwa;
(ii). Kusimamia maandalizi ya nyenzo mahsusi za tathmini za taasisi kulingana na maelekezo ya Mwongozo;
(iii). Kusimamia utekelezaji wa tathmini zilizoidhinishwa kulingana na wakati uliopangwa;
(iv). Kusimamia matumizi ya matokeo ya tathmini kwa lengo la kufanya maboresho, kufanya maamuzi yenye ushahidi na kujifunza.
(v). Kudhibiti ubora wa data na tathmini zainazotekelezwa na taasisi;
(vi). Kuandaa taarifa za tathmini za taasisi na kuziwasilisha katika wizara husika.

## 4.6 Ofisi ya Rais Tawala za Mikao na Serikali za Mitaa (TAMISEMI)

OR-TAMISEMI ni Ofisi simamizi kwa Sektretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Katika kuwezesha utekelezaji wa tathmini husika, OR-TAMISEMI itawajibika na:

(i). Kusimamia utekelezaji wa Mwongozo huu katika kila Sektretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;
(ii). Kusimamia ubora wa tathmini katika Sektretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;
(iii). Kuhakikisha vigezo vya tathmini vinafuatwa kulingana na aina ya tathmini zinazotekelezwa.
(iv). Kusimamia uchambuzi na uchakataji wa tathmini zitakazotekelezwa katika ngazi ya Mkoa na Halmashauri
(v). Kusimamia maadalizi ya mpango wa tathmini wa mwaka;
(vi). Kusimamia utekelezaji wa mapendekezo yanayotokana na matokeo ya tathmini hizo; na
(vii). Kusimamia na kuratibu ujenzi wa uwezo wa kufanya tathmini za afua mbalimbali

### 4.7 Sekretarieti za Mikoa

Idara zinazohusika na shughuli za U&T zitawajibika kuhakikisha tathmini zinatekelezwa katika halmashauri zote za mkoa husika. Idara hizo zitawajibika na:-

(i). Kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Tathmini ndani ya Mkoa husika
(ii). Kusimamia ubora wa data zitokanazo na tathmini zinazofanyika katika Mkoa husika
(iii). Kudhibiti ubora wa tathmini zinazotekelezwa na sekretarieti ya mkoa na halmashauri zake; na
(iv). Kusimamia maandalizi ya taarifa za tathmini na kuwasilisha OR – TAMISEMI kwa ajili ya kuidhinishwa na kuwasilishwa OWM - SBU.

### 4.8 Mamlaka za Serikali za Mitaa

Idara zinazohusika na shughuli za U&T zitawajibika kuhakikisha tathmini zinafanyika kama ilivyopangwa katika halmashauri zote za mkoa husika ikiwa ni pamoja na kata na mtaa/kijiji. Idara hizo zitawajibika na:

(i). Kusimamia matumizi ya matokeo ya tathmini katika ngazi ya Halmashauri katika mipango, bajeti na maamuzi ya viongozi.
(ii). Kusimamia maandalizi ya taarifa za tathmini na kuwasilisha sekretarieti ya mkoa.

**Prime Minister's Office**
**Policy, Parliament and Coordination**

Government City, Mtumba
P.O. Box 980
Dodoma, Tanzania
Email: ps@pmo.go.tz
www.pmo.go.tz

**Ofisi ya Waziri Mkuu**